



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



YAH: TAARIFA KWA UMMA  
WAKALA AHUKUMUMIWA KWA KUTUMIA MADARAKA YAKE VIBAYA

Mahakama ya wilaya ya Bukombe Mkoani Geita imemtia hatiani na kumuhukumu aliyekuwa wakala wa ukusanyaji wa mapato ya halmashauri kwa kutumia mfumo wa ( POS) Bw NELSON JIBALO MDULA aliyekuwa anakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi namba 28848/2024 kulipa faini ya TZS 100,000/= au kifungo cha miezi 6 na kulipa Fedha za Halmashauri kiasi cha TZS 1,727,200/= kwa kosa la ubadhilifu na ufujaji kinyume na kifungo cha 28( 1) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa [Sura ya 329 Marejeo ya mwaka 2022]

Mshtakiwa alifikishwa Mahakamani October 08, 2024 mbele ya Hakimu mwandamizi wa Mahakama ya wilaya ya Bukombe Mhe. BAHATI CHITEPO na kusomewa Mashtaka na wakili wa serikali mwandamizi wa TAKUKURU Bw. Chali Kadegehe

Wakili alieleza Mahakama kwamba kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 Mshtakiwa alifanya ubadhilifu na ufujaji kwa kukusanya Fedha kwa kutumia POS mashine kama wakala na kushindwa kuwasilisha Fedha hizo kwenye akaunti ya Halmashauri na kuzitumia kwa manufaa yake mwenyewe kiasi cha TZS 1,727,200/=

Mshitakiwa amekiri kosa kwa (Mfumo wa Plea bargaining) na Mahakama imeamuru kulipa faini ya TZS 100,000/- au kutumikia kifungo cha miezi 6 na kurejesha fedha za halmashauri kiasi cha TZS 1,727,200/= Ambapo mshtakiwa amelipa faini ya TZS 100,000/= na kurejesha Fedha za Halmashauri kiasi cha TZS 1,727,200/= .

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Geita Bw. Azza Mtaita ametoa wito kwa wananchi kutoa taarifa za vitendo mbalimbali vya Rushwa wakati wowote wanapohisi au kuona vinatendeka katika idara mbalimbali za serikali

*Imetolewa na:*  
  
Azza E. Mtaita  
**MKUU WA TAKUKURU**

*Borua zote zitumwe kwa Mkuu wa Takukuru, Mtaa wa Nyanza S.L.P 38 GEITA, Simu Kambari (028) 2520004.  
Barua Peper/bcgeita@pccb.go.tz, Tovuti:www.pccb.go.tz, Simu ya Bure 113, Instagram: Takukuru Tz,  
Twitter:TAKUKURUTZ Online Tv:TAKUKURU TV*